Kiambatisho Cha I: Barua ya Human Rights Watch kwa Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, Agosti 9, 2016

Mhe. Ummy Ally Mwalimu, Waziri
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wazee na Watoto
Kivukoni Front
S.L.P 3448
Dar es Salaam
Tanzania

Kwa njia ya barua pepe: umwalimu@gmail.com; umwalimu@parliament.go.tz

Kupitia kwa Katibu Mkuu: ps@mcdgc.go.tz

Yah: Vilainishi vya maji na Uzuiaji wa VVU

Mpendwa Mhe. Waziri Ummy Mwalimu,

Tunaandika barua hii kwa niaba ya Human Rights Watch, shirika la kimataifa ambalo linanakili wazi hati za ukiukwaji wa haki wa kibinadamu katika mataifa zaidi ya 90 kote ulimwenguni na inafanya kazi na serikali kuhakikisha kwamba haki za kibinadamu zinafuatwa na kuimarishwa. Kwa miaka ya hivi karibuni, tumeripoti matukio ya ukiukwaji wa haki wa kibinadamu kwa makundi yaliyo hatarini nchini Tanzania zikiwemo haki za wajane za urithi, ndoa za utotoni, na ajira kwa watoto wadogo katika sekta ya madini. Kuhusu ubaguzi dhidi ya makundi maalum yaliyoathirika na VVU, tumelenga wafanyabiashara ya ngono, wanaume wanaofanya mapenzi na waume wenzao na wale ambao ni waraibu wa madawa ya kulevya.

Tunaandika kuelezea wasiwasi wetu kuhusu uamuzi wa hivi karibuni wa serikali ya Tanzania kupiga marufuku ugawaji wa vilainishi vya maji kwa wanaume ambao wanashiriki ngono na wanaume wenzao, kama ilivyoelezwa katika waraka wa Wizara ya

Afya tarehe 19 Julai[292] na kufafanuliwa zaidi katika chapisho la kwenye ukurasa wako Facebook la tarehe 24 Julai. Maamuzi haya yanaonyesha wazi nia ya kupinga kukuzwa kwa mahusiano ya jinsia moja."

Kama ambavyo utakuwa unafahamu Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Tanzania kuhusu VVU /UKIMWI ambao ulichapishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu mwaka wa 2013 na ambao unatekelezwa hadi 2018, na ambao unahimiza kuongezeka kwa ufikiaji wa vilainishi vya maji kwa wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao na wafanyabiashara ya ngono.[293] Miongozo ya kitaifa kuhusu mipango ya VVU kwa makundi maalum, iliyochapishwa na wizara yako mnamo Septemba 2014 inathibitisha kwamba, "kuongezwa kwa upatikanaji, ufikiaji, uwezo wa kumudu bei, na matumizi ya …vilainishi vinayoambatana vyema na kondomu miongoni mwa watu kutoka makundi maalum kupitia kwa mipango ya usambazaji inayowalenga ni kiungo muhimu cha kupambana na VVU."[294]

Vilainishi vya maji vimedhihirika kuwa vyenye uwezo mkubwa katika kusaidia kupunguza ueneaji wa VVU. Kuna uwezekano mkubwa wa mipira ya kiume kupasuka wakati ambapo wapenzi wanafanya mapenzi kupitia njia ya haja kubwa bila kutumia vilainishi, au wanapotumia vilainishi vya mafuta kama vile Vaseline. Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) linaelezea "mpango kamilifu wa mipira ya kiume na vilainishi" kama muhimu kwenye huduma za VVU miongoni mwa makundi maalum.[295] Miongozo ya UNAIDS iasema kwamba "Miradi inapaswa kuhakikisha kwamba vilainishi vya maji au vya silika vinakuwepo pamoja na kondomu," huku ikizingatiwa kwamba vilainishi "vina umuhimu wa hali ya juu kwa wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao, wafanyabiashara ya ngono na wanawake waliojifungua."[296]

Kama ulivyobaini, maambukizi ya VVU miongoni mwa wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao nchini Tanzania ni ya juu kuzidi watu wengine kwa jumla. Kwa mujibu

---

[292] Habari 360, "Hili Hapa Tamko la Wizara ya Afya Kuhusu Matumizi na Usambazaji wa Vilainishi," Julai 19, 2016, http://www.habari360.com/2016/07/hili-hapa-tamko-la-wizara-ya-afya.html?m=0.

[293] Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Waziri Mkuu, *Mkakati wa Taifa wa Tatu wa Mapambano Dhidi ya VVU na UKIMWI (2013/14 – 2017/18)*, Novemba 2013, uk. 39, uk. 47.

[294] Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Tanzania Bara, *Muongozo Jumuishi wa Taifa wa KUpambana na VVU kwa Makundi Maalum,* http://www.emtct-iatt.org/wp-content/uploads/2016/01/Tanzania_KP_Comprehencive_Guideline_sept_29th_2014.pdf, Septemba 2014, uk. 25.

[295] Shirika la Afya Duniani, Kinga ya VVU, Kipimo, Tiba na Huduma kwa Makundi Maalum: Miongozo Jumuishi, Julai 2014, http://apps.who.int/iris/bitstream/10665/128049/1/WHO_HIV_2014.8_eng.pdf?ua=1&ua=1, uk. 3.

[296] UNAIDS, Programu ya Mipira ya Kiume na Vilainishi katika nchi zenye maambuki makubwa ya VVU, Ujumbe wa Mwongozo, 2014, http://www.unaids.org/sites/default/files/media_asset/condoms_guidancenote_en.pdf, uk. 5-8.

wa Tume ya UKIMWI Tanzania (TACAIDS), taasisi ya serikali, maambukizi miongoni mwa wananchi kwa jumla ilikuwa ni aslilimia 5.1 mwaka wa 2012, ilihali miongoni mwa MSM ilikuwa ni kati ya asilimia 12 na asilimia 41.[297]

Kiwango hiki cha juu cha watu wanaoambukizwa kinaonyesha kuwa serikali ya Tanzania inapaswa kuongezea juhudi, wala siyo kupunguza, kufikia MSM na kuhakikisha kuwa wamejumuishwa kikamilifu katika programu za kuzuia VVU - na kwamba hawakumbwi na unyanyapaa na ubaguzi wakati wa kupata huduma. Utafiti uliofanywa miaka ya 2012-2013 na shirika la Human Rights Watch na shirika la Wake Up Step Forward Coalition, mtandao wa mashirika yanayofanya kazi kwa MSM, uligundua kuwa ubaguzi na unyanyasaji huzuia MSM, pamoja na wafanyabiashara ya ngono na wanaojidunga dawa za kulevya, kupata huduma za serikali za kutosha.[298] UNAIDS imethibitisha kwamba unyanyapaa na ubaguzi huchangia kuwepo kwa viwango vya juu vya maambukizi VVU miongoni mwa makundi maalum, na kwamba ni shart nchi zishughulikie unyanyapaa na kurekebisha sera na sheria za kibaguzi iwapo wangetaka kuona maambukizi ya VVU yakipungua.[299]

Ukosefu wa vilainishi vya maji ni baadhi ya sababu zinazochangia kuongezeka kwa maambukizi ya VVU miongoni mwa wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao na wafanyabiashara ya ngono kulingana na utafiti wa Human Rights Watch na WASO. Takribani wanaume wote wanaofanya ngono na wanaume wenzao waliohojiwa na Human Rights Watch na WASO mwaka wa 2012 na 2013 walisema kuwa hawajui wapi pa kununua vilainishi vya maji na wengine hawana kipato cha kutosha kununua katika maduka ya madawa. Kulingana na “Lester,”ambaye ni shoga mjini Arusha anasema “Ni rahisi kupata mipira ya kiume kuliko vilainishi. Unaweza kwenda maduka kama matano ukitafuta KY [aina ya vilainishi vilivyotengezwa na maji] bila kupata. Kwa hivyo natumia [vilainishi vya mafuta] Vaseline.” Katika mji wa Mbeya, “Christian,”ambaye ni mfanyabiashara wa ngono wa kiume, aliambia Human Rights Watch kwamba alikuwa amelazimika kutumia vilainishi vya mafuta kwa sababu vilainishi vya maji havipatikani.

---

[297] Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ripoti ya Maendeleo ya Nchi ya Mapambano ya Dunia Dhidi ya UKIMWI, Machi 31, 2014, http://www.unaids.org/sites/default/files/country/documents/TZA_narrative_report_2014.pdf, uk. 13.

[298] Human Rights Watch na WASO, “*Tuchukulie Kama Binadamu”: Ubaguzi Dhidi ya Wafanyabiashara ya Ngono, Walio katika Makundi madogo ya Kingono na Kijinsia, na Watumia Dawa za Kulevya Tanzania*, Juni 18, 2013, https://www.hrw.org/report/2013/06/18/treat-us-human-beings/discrimination-against-sex-workers-sexual-and-gender.

[299] UNAIDS, Programu za Muhimu Katika Kupambana na Unyanyapaa na Ubaguzi na Kuongeza Haki katika Mapambano ya Kitaifa dhidi ya VVU, Ujumbe wa Mwongozo, 2012, http://files.unaids.org/en/media/unaids/contentassets/documents/document/2012/Key_Human_Rights_Programmes_en_Mei 2012.pdf.

Lester na Christian wote wanajua kuwa matumizi ya vilainishi vya mafuta kama vile Vaseline yana uwezo wa kupasua mpira wa kondomu wakati wa ngono na kuongezea hatari ya kupata VVU lakini hawakuwa na mbadala mwingine wowote.[300]

Mpango wa hivi karibuni wa vilainishi wa mashirika yasiyo ya kiserikali nchini Tanzania ulikuwa na lengo la kukatua mwanya huu mkubwa uliopo wa upungufu na kufanya vilainishi vya maji kupatikana kwa wingi kwa wanaume kama vile Lester na Christian – lengo ambalo asasi za kiraia zinazofanya kazi ya VVU Tanzania zimelitambua kama la kupewa kipaumbele. Mkutano ulioandaliwa na kuongozwa na AIDS Accountability mwezi wa Mei mwaka wa 2014, Wanachama 78 asasi za kiraia nchini Tanzania walikutana na kuweka muhtasari mambo ya msingi yake na vipaumbele vya mradi wa Global Fund kazi ya kuangazia VVU/UKIMWI nchini Tanzania; na wakaorodhesha "huduma rafiki za daraja la chini kwa jamii ya makundi maalum," ikiwemo upatikananji wa kondomu na vilainishi kama kipaumbele cha pili muhimu cha kuwekeza rasilimali ya Global Fund.[301] Mashirika haya yalitambua kwamba usambazaji wa vilainishi vya maji hauhusiani na "ukuzaji wa mapenzi ya jinsia moja" – unahusu suala muhimu la kuokoa maisha.

Kama serikali ya Tanzania imedhamiria kumaliza kuenea kwa VVU, inapaswa kupigia chepuo matumizi ya vilainishi vya maji, siyo kuweka vikwazo. Tanzania ni mwanachama wa Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni, ambao unalinda haki ya viwango vya juu iwezekanavyo vya afya. Kukataa mitazamo inayotegemea ushahidi ya kuzuia VVU miongoni mwa makundi yaliyotengwa, na kubagua katika utoaji wa ufikiaji wa huduma muhimu za afya, ni ukiukaji wa haki hiyo.[302] Tanzania inavyoendelea kuweka vikwazo katika usambazaji wa vilainishi kwa makundi maalum, ndivyo kunaongezeka uwezekano wa kuona idadi za juu za maambukizi – na vifo vinavyoweza kuzuiliwa – miongoni mwa makundi haya.

Tunakuhimiza sana kuhakikisha ya kwamba mtazamo wa Tanzania kwa vilainishi vya maji unaongozwa na viwango bora vya utendaji ambavyo vimewekwa na mashirika ambayo

---

[300] Human Rights Watch na WASO, "*Tuchukulie Kama Binadamu": Ubaguzi Dhidi ya Wafanyabiashara ya Ngono, Walio katika Makundi madogo ya Kingono na Kijinsia, na Watumia Dawa za Kulevya Tanzania*, uk. 80-81.

[301] Shirika la AIDS Accountability International, "Tanzania Civil Society Priorities Charter: An Advocacy Roadmap for the Global Fund to fight AIDS, Tuberculosis and Malaria New Funding Model," Mei 2014, http://www.aidsaccountability.org/wp-content/uploads/2014/02/Tanzania-Civil-Society-Priorities-Charter.pdf.

[302] Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu, KHUJT (CESCR) Maoni ya Jumla No. 14: Haki ya Kupata Huduma Bora Zaidi za Afya (Ibara. 12), Iliyopitishwa katika Mkutano wa Ishirini na Mbili wa Kamati ya Haki ya Uchumi, Jamii na Tamaduni, tarehe 11 Agosti 2000, http://www.ohchr.org/Documents/Issues/Women/WRGS/Health/GC14.pdf, aya. 12(b).

yana utaalamu na uzoefu wa miongo katika kushughulikia VVU, kama vile UNAIDS na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), na kuweka hakikisho la kudumisha haki ya kufikia kiwango cha juu zaidi kiwezekanacho cha afya.

Tutashukuru tukipata majibu yako juu ya hii barua, kutujulisha hatua ambazo serikali ya Tanzania itachukua kuhakikisha mashirika yasiyo ya kiserikali yanaweza kuendeleza na kupanua usambazaji wa vilainishi maji kwa jamii ya watu wa makundi maalumu.

Tafadhali tuma majibu kwetu kupitia kwa Mtafiti Mkuu, Bi Neela Ghoshal, Kupitia [redacted]

Wako waaminifu,

Diederik Lohman
Kaimu Mkurugenzi, Mradi wa Afya na Haki za Binadamu

Liesl Gerntholtz
Kaimu Mkurugenzi – Kitengo cha Afrika

Graeme Reid
Mkurugenzi, Programu ya Haki za LGBT

Nakala kwa:
Ofisi ya Rais
Kwa njia ya barua pepe: ikulu@ikulu.go.tz

Ofisi ya Waziri Mkuu
Kwa njia ya barua pepe: ps@pmo.go.tz

Kamati ya Kulinda Haki za Watu Wanaoishi na VVU na Walio Kwenye Hatari, Wanyonge, Waliohatarini na Walioathirika na VVU,
(Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu)
Kwa njia ya barua pepe: au-banjul@africa-union.org

Mratibu Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu Kiwango cha juu Kuzidi cha Afya Kinachowezekana
Kwa njia ya barua pepe: srhealth@ohchr.org

UNAIDS
Kwa njia ya barua pepe: aidsinfo@unaids.org

Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (The Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis and Malaria)
Kwa njia ya barua pepe: info@theglobalfund.org